**MAELEZO YA USULI KUTOKA KWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA, MHE. DKT. SELEMANI SAIDI JAFO (MB.) KATIKA HAFLA YA UZINDUZI WA SERA YA TAIFA YA MAZINGIRA, 12 FEBRUARI, 2022, DODOMA**

**==================================**

***Mgeni Rasmi, Mhe. Dkt Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Waheshimiwa Mawaziri;***

***Waheshimiwa Manaibu Mawaziri;***

***Mhe. Anthony John Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;***

***Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu;***

***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;***

***Waheshimiwa Wabunge;***

***Waheshimiwa Madiwani;***

***Viongozi mbalimbali wa Vyama vya Siasa;***

***Viongozi wa Dini;***

***Washirika wa Maendeleo;***

***Asasi za Kiraia;***

***Sekta Binafsi***

***Ndugu Wanahabari;***

***Mabibi na Mabwana;***

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi,***

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa tukiwa na afya njema. Aidha, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Taifa letu kwa busara na hekima na tunamwombea kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake. Vilevile, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wako pamoja na maelekezo yako adhimu yanayotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi ili kuhakikisha mazingira yetu yanalindwa na nchi yetu inaendelea kuwa sehemu salama ya kuishi.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi,***

Mbele yako ni wageni waalikwa waliojumuika nasi siku ya Ieo katika hafla hii, hivyo basi, napenda nitambue uwepo wa Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu wakuu, Manaibu Katibu Mkuu kutoka Wizara mbalimbali za kisekta na Wakuu wa Taasisi mbalimbali za umma na sekta binafsi, Wajumbe Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira na Kamati ya Maliasili na Utalii.

Vilevile, napenda nitambue uwepo wa wakuu wa Mikoa na Wilaya; Wabunge; Madiwani; Viongozi wa Vyama vya Siasa; Viongozi wa Taasisi za Dini; Kamati ya Kampeni Kabambe ya Usafi ya Hifadhi ya Mazingira; Wadau wa Maendeleo; Mashirika yasiyo ya Kiserikali; Sekta

Binafsi; Taasisi za Elimu ya Juu; na wadau mbalimbali wanaojishughulisha na masuala ya hifadhi ya mazingira.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi,***

Kufuatia changamoto zilizoelezwa na Katibu Mkuu kuhusu Sera ya Taifa ya Mazingira mwaka 1997 na ili kufanikisha azma ya Serikali ya uhifadhi na usimamizi endelevu wa mazingira nchini, Ofisi imeandaa Sera mpya ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 ambayo utaizindua leo.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi,***

Sera utakayoiziundua leo imeweka malengo na matamko mahususi ya Kisera yatakayowezesha kukabiliana na changamoto za mazingira nchini kwa ufanisi mkubwa. Aidha, Sera hii imezingatia fursa za kiuchumi katika hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini ambazo hazikutambuliwa na Sera ya awali. Fursa hizo ni kama vile:

i. Urejelezaji wa taka ambao unapunguza gharama za udhibiti wa taka na kuongeza kipato;
ii. Utengenezaji wa bidhaa rafiki kwa mazingira kama Mifuko mbadala ya plastiki, Majiko banifu na Mkaa mbadala; na
iii. Biashara ya hewa ukaa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Vilevile, Sera hii imezingatia kuwepo kwa mipango mipya ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Mpango Elekezi wa Miaka Kumi na Tano

(2011/12 – 2025/26); Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22- 2025/26); Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030) na Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi,***

Kama ulivyoagiza, uzinduzi wa Sera siku ya leo ulitanguliwa na wiki ya uzinduzi wa Sera iliyoanza tarehe 7 Februari 2022 hadi kufikia leo siku ya kilele cha uzinduzi. Katika wiki hii, Ofisi yako kwa kushirikiana na Jiji la Dodoma, taasisi, sekta binafsi, wafanyabiashara na wananchi walishiriki katika kufanya shughuli mbalimbali zenye lengo la hifadhi na usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma. Katika shughuli za upandaji miti zilizofanyika katika Wiki ya Uzinduzi wa Sera katika Jiji la Dodoma jumla ya miti 3,100 ilipandwa. Aidha, zoezi la upandaji miti lilifanyika katika maeneo mengine ya Mkoa wa Dodoma ambapo miche ya miti 450,000 imesambazwa na kupandwa katika Halmashauri za Wilaya ya Kiteto, Bahi, Kongwa, Mpwapwa, Chamwino na Dodoma Jiji. Hivyo jumla ya miti iliyopandwa ni 453,100.

Dhumuni la kuwepo kwa shughuli hizo ni pamoja na: - Kurejesha hali ya asili ya mazingira iliyoharibika kutokana na shughuli za kibinadamu; Kuwa na mazingira safi ili kuboresha afya ya jamii na Kuelimisha jamii kuhusu utenganishaji taka kwa ajili ya udhibiti wa taka ngumu na kuwezesha urejelezaji wa taka kwenye bidhaa na huduma mbalimbali. Shughuli zilizotekelezwa katika Wiki ya Uzinduzi wa Sera ni pamoja na: -

i. Upandaji miti Jijini Dodoma katika maeneo yafuatayo: -

- Medeli, siku ya Jumatatu tarehe 07/02/2022
- Iyumbu, siku ya Jumanne tarehe 08/02/2022
- Isern, siku ya Jumatano tarehe 09/02/2022
- Maeneo ya barabara inayoanzia Chimwaga, Chuo Kikuu cha Dodoma kuelekea barabara ya Dodoma Dar es Salaam (Leo siku ya Uzinduzi)

ii. Kufanya usafi pembezoni mwa barabara inayoanzia Shule ya Martin Luther hadi Wajenzi kupitia Nzuguni, Ilazo, Ipagala na Area C tarehe 08 Februari, 2022 siku ya Jumanne;

iii. Kutoa elimu kuhusu utenganishaji wa taka na kufanya Usafi katika soko la Chang'ombe tarehe 10 Februari, 2022 siku ya Alhamisi;

iv. Utoaji wa Elimu ya Mazingira kwa wananchi na wadau kupita vyombo vya habari.

Hivyo, ni matumaini yangu kuwa ari hii itaendelea kama sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 utakayoizindua leo hii na hatimaye kufanikisha azma ya Serikali ya uhifadhi wa mazingira na kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

Baada ya kusema hayo napenda sasa kwa heshima na taadhima kukukaribisha uweze kuhutubia hadhara hii na kisha kuzindua Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 pamoja na Mkakati wa utekelezaji wake.

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi Karibu sana***